

## TAARIFA KWA UMMA

## MUHIMU: Taasisi ya Afya Ifakara Inazingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Weledi Kwenye Mchakato wa Ajira

> *TAHADHARI: Taasisi Yetu Haihusiki na Mtu au Kikundi Kinachotumia Jina Letu Kufanya Utapeli kwa Kisingizio cha Kutoa Ajira*

<p>F37-VAN-v20.1</p> <p>ISO 9001:2015 certified</p> <p><b>VACANCY ANNOUNCEMENT</b></p> <p> IFAKARA HEALTH INSTITUTE research   training   services</p> <p>#IfakaraJobs</p>	<p>Matangazo yote ya ajira kwenye Taasisi ya Afya Ifakara hutangazwa kwenye:</p> <p>&gt;&gt;Tovuti: <a href="http://www.ihl.or.tz">www.ihl.or.tz</a></p> <p>Mitandao ya kijamii (Facebook &amp; Twitter):</p> <p>&gt;&gt;Handle: <a href="https://www.facebook.com/ifakarahealth">@ifakarahealth</a></p> <p>Maombi yote ya kazi hutumwa:</p> <p>&gt;&gt;Email: <a href="mailto:recruitment@ihl.or.tz">recruitment@ihl.or.tz</a></p> <p>Husimamiwa na:</p> <p>&gt;&gt;Kitengo cha <a href="#">Rasilimali Watu, Dar es Salaam.</a></p>
---	--

Octoba 12, 2022 – IFAKARA. Taasisi ya Afya Ifakara inatoa tahadhari kwa umma kuhusiana na kuzuka kwa watu au vikundi vya watu vinavyotumia jina la Taasisi yetu kufanya utapeli kwa kuwaahidi ajira. Tunapenda ifahamike wazi kwa umma kuwa Taasisi yetu inaajiri kwa mujibu wa sheria na kanuni za ajira zilizowekwa na mamlaka husika nchini Tanzania. Halikadhalika, Taasisi imejiwekea miongozo yake yenyewe inayosimamia taratibu na michakato yote ya ajira kwa kuzingatia weledi.

Hivyo basi, Taasisi ya Afya Ifakara haihusiki kwa namna yotote ile na mtu, watu au kikundi kinachotapeli watu kwa kuahidi kuwapa ajira huku kikiwatoza fedha au kwa namna yoyote ile isiyofaa. Ifahamike kwa umma kuwa, nafasi zote za ajira kwenye Taasisi yetu hutangazwa kupitia tovuti na mitandao ya kijamii ya Taasisi yetu, na pale tunapona ipo haja, matangazo hayo hutolewa kwenye vyombo rasmi vya habari kwa uwazi na weledi.

Mwisho, tunapenda kuutahadharisha umma kujiepusha na matapeli hao na kutumia vyanzo vyetu rasmi vya kutoa matangazo ya ajira tulivyoainisha hapo juu. Aidha, Taasisi yetu tayari inashirikiana na vyombo vya Usalama, ikiwemo Jeshi la Polisi, kuhakikisha kuwa utapeli huu unakomeshwa na sheria inachukua mkondo wake dhidi ya mtu, watu au kikundi kinachojihusisha vitendo hivyo.

### Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano,

Taasisi ya Afya Ifakara,

#5 Mtaa wa Ifakara Kitalu Namba 463 Mikocheni | Kinondoni, Dar es Salaam

+255 222 774 756 | [communications@ihl.or.tz](mailto:communications@ihl.or.tz)

[info@ihl.or.tz](mailto:info@ihl.or.tz) | [www.ihl.or.tz](http://www.ihl.or.tz)

### Tawi la Ifakara

Eneo la Mlabani  
S.L.P 53 Ifakara  
Simu: +255232931572

### Ofisi ya Dar es Salaam

#5 Mtaa wa Ifakara Kitalu 463 Mikocheni  
S.L.P 78,373 Dar es Salaam  
Simu: +255222774756

### Bagamoyo Branch

Eneo la Hospitali ya Wilaya  
S.L.P 74 Bagamoyo  
Simu: +255232440065